OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

Simu Na. 027-2530022
Barua pepe:ded@hanangdc.go.tz
Tovuti:www.hanangdc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Hanang,
2 Barabara ya Amani,
S.L.P. 2,
27382 Ganana – Hanang,
MANYARA.

**27/06/2025**

# TANGAZO TANGAZO TANGAZO

**Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang anawatangazia wananchi wote kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang inauza viwanja vilivyopo katika eneo la Mpango Mji wa makazi mapya ya kisasa Warret – Gidagamowd na wananchi wote mnatangaziwa uwepo wa viwanja hivyo na kwa yeyote anayehitaji anatakiwa kutuma maombi kwa kujaza fomu maalum ambayo inapatikana Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya – Idara ya Ardhi. Unatakiwa kutuma maombi yako ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili, - yaani tarehe 27/06/2025 hadi tarehe 11/07/2025.**

**Viwanja hivi tayari vimezungukwa na makazi ya watu wapatao 700 (Waathirika wa mafuriko ya Desemba 3, 2023 waliofadhiliwa nyumba 109) na vipo katika eneo ambalo tayari lina Miundombinu yote muhimu ikiwemo Barabara, Umeme, Shule ya Msingi na Sekondari, Maji safi na salama, Zahanati na Majengo ya Ibada. Masharti yafuatayo yazingatiwe kwa mwombaji:-**

**(I)** Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**(II)** Awe na umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
**(III)** Mwombaji aoneshe matumizi ya kiwanja anachoomba
**(IV)** Fomu ya maombi ibandikwe picha ndogo ya rangi ya mwombaji pamoja na uthibitisho wa uraia (NIDA). Fomu ya maombi iambatane na malipo ya Tsh.20,000.00 ambayo haitarejeshwa, endapo mwombaji atakosa kiwanja, (Control Namba utapewa na Afisa wa Ardhi).
**(V)** Awe na uwezo wa kukiendeleza kiwanja kwa mujibu wa masharti ya umiliki.
**(VI)** Awe na uwezo wa kulipia kiwanja kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza atalipa 60% na awamu ya pili 40% kwa muda utakaopangwa.
**(VII)** Kiwanja kinauzwa kwa Tsh. 4,000/= kwa mita za mraba kwa kiwanja cha makazi na Tsh. 5,000/= kwa mita kwa kiwanja cha makazi na biashara.
**(VIII)** Awe tayari kusaini Mkataba Maalum wa Makabidhiano ya Kiwanja, baada ya malipo kwa kutumia Control Namba.

**Tafadhali usomapo tangazo hili mtaarifu na mwenzako.**

**"Tujenge Hanang yetu kwa maendeleo ya wote"**

**Teresia A. Irafay**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA
HANANG